NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED



MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)

JARIDA LA MTANDAONI

# USAJILI WA KAYA ZISIZO NA UWEZO NA BIMA YA AFYA KWA WOTE

MEI
2026

#Bima ya Afya kwa Wote, **Jiunge Sasa !**

0800 787800 www.nhif.or.tz nhiftz

# Yaliyomo


**Manyara** 01
*Kaya 3,998 Zisizo na Uwezo Zafikiwa Manyara*

**Singida** 02
*Kaya 7,313 Zisizo na Uwezo Singida zafikiwa Bima ya Afya*

**Kigoma** 03
*Asilimia 66 ya Kaya Zisizo na Uwezo Kigoma Zasajiliwa Bima ya Afya*

**Tanga** 04
*Kaya 13,100 Zisizo na Uwezo Tanga zasajiliwa bima ya afya*

**Katavi** 05
*Asilimia 55 ya Kaya Zisizo na Uwezo Zafikiwa Katavi*

**Kagera** 06
*Kaya 9,908 Zisizo na Uwezo Kagera Zafikiwa*

**Tabora** 07
*Asilimia 52 ya Kaya Zisizo na Uwezo Tabora zafikiwa Bima ya Afya*

**Iringa** 08
*Asilimia 66 ya Kaya Zisizo na Uwezo Iringa zafikiwa Bima ya Afya*

**Dar es Salaam** 09
*Asalimia 57 ya Kaya Zisizo na Uwezo Dar es Salaam zasajiliwa Bima ya Afya*

**Simiyu** 10
*Asilimia 56 ya Kaya Zisizo na Uwezo zasajiliwa Simiyu*

**Shinyanga** 11
*Asilimia 54 ya Kaya Zisizo na Uwezo Shinyanga zasajiliwa Bima ya Afya*

**Pwani** 12
*Asilimia 53 za Kaya Zisizo na Uwezo Pwani zasajiliwa Bima ya Afya*

**Morogoro** 13
*Asilimia 70 ya Kaya Zisizo na Uwezo Morogoro zasajiliwa Bima ya Afya*

**Geita** 14
*Asilimia 64 ya Kaya Zisizo na Uwezo zafikiwa Bima ya Afya kwa Wote*

**Dodoma** 15
*Bima ya Afya Kwa Wote Yaacha Kicheko Dodoma*

**Arusha** 16
*Asilimia 43 ya Kaya Zisizo na Uwezo Arusha zasajiliwa Bima ya Afya*

**Ruvuma** 17
*Kaya 5,154 zisizo na uwezo Ruvuma zasajiliwa Bima ya Afya*

**Rukwa** 18
*Asilimia 66 ya Kaya Zisizo na Uwezo Rukwa Zasajiliwa Bima ya Afya*

**Lindi** 19
*Kaya 1,570 zisizo na uwezo Lindi zasajiliwa Bima ya Afya*

**Mwanza** 20
*Asilimia 71 ya Kaya Zisizo na Uwezo Mwanza zasajiliwa Bima ya Afya*

**Njombe** 21
*Njombe kuwa na Uhakika wa Matibabu*

**Songwe** 22
*Songwe wafikiwa Bima ya Afya kwa Wote*

**Mbeya** 23
*Asilimia 60 ya Kaya Zisizo na Uwezo Mbeya zasajiliwa Bima ya Afya*

**Mtwara** 24
*Asilimia 75 ya Kaya Zisizo na Uwezo Mtwara zasajiliwa Bima ya Afya*

**Kilimanjaro** 25
*Asilimia 62 ya Kaya Zisizo na Uwezo Kilimanjaro Zafikiwa Bima ya Afya kwa Wote*

**Mara** 26
*Mara kunufaisha wananchi 17,205 Bima ya Afya kwa Wote*

# Utangulizi

Mwezi Februari 2026, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulianza zoezi la uhakiki na utoaji wa kadi za bima ya afya kwa wanufaika kutoka katika kaya zisizo na uwezo ambazo zimelipiwa na Serikali kwa Awamu ya kwanza. Zoezi lililenga kuhakiki na kutoa kadi kwa kaya 276,004 na wanufaika 1,206,319 katika mikoa yote Tanzania Bara katika awamu ya kwanza.

Ili kuhakikisha zoezi hili linakuwa na ufanisi mkubwa, Mfuko ulishirikiana na wataalam kutoka Wizara ya Afya, TAMISEMI na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ngazi ya Kitaifa kusimamia zoezi la uhakiki.

Aidha Mfuko ulitoa taarifa ya kuanza kwa zoezi kwa Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) na kuwaomba kutoa taarifa kwa Viongozi wa Mikoa na Wilaya kuhusu kuanza kwa zoezi hilo na kuomba ushirikiano kutoka kwa viongozi husika. Viongozi hao ni pamoja na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri;

Mfuko uliwashirikisha Wakuu wa Mikoa na Wilaya katika uhamasishaji wa walengwa kujitokeza kwa wingi katika zoezi la uhakiki na utoaji wa kadi. Uhamasishaji ulifanyika kupitia vyombo vya habari na kutembelea vituo ambavyo mazoezi yamekuwa yakitekelezwa;

Mbali na hayo, pia vilifanyika vikao vya maandalizi baina ya maafisa wa Mfuko/ TAMISEMI / Wizara ya Afya na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Halmashauri, kutolewa kwa elimu za zoezi katika mabaraza ya madiwani katika Halmashauri mbalimbali pamoja na ushirikishwaji wa Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji wa Kijiji, Waratibu wa TASAF na Waratibu wa Bima katika halmashauri mbalimbali.

Matokeo ya zoezi hilo ambalo lilifanyika katika Mikoa yote Tanzania Bara. Halmashauri 144 zimefikiwa kati ya 184 sawa na asilimia 78 ya lengo. Idadi ya kaya 106,321 zimehakikiwa na kupatiwa kadi kati ya kaya 276,004 zilizolengwa sawa na asilimia 40.

Jarida hili linaangazia utekelezaji wa zoezi la usajili wa Kaya zisizo na uwezo kwa kila mkoa.

# Manyara

## Kaya 3,998 Zisizo na Uwezo Zafikiwa Manyara

Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkoa wa Manyara imefanikiwa kusajili jumla ya Kaya 3,998 sawa na asilimia 31 zisizo na uwezo ambazo zililengwa kunufaika na huduma za Bima ya Afya kupitia mpango wa Serikali wa kuhudumia kaya zisizo na uwezo.

Mkoa huo una jumla ya wanufaika 56,264 waliolengwa kwenye mpango huu ambapo jumla ya wanufaika 11,899 tayari wametambuliwa, kusajiliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu.

Zoezi hili limeongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara kwa ushirikiano wa karibu na Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani humo. Wadau hao wamejipanga kuhakikisha kuwa walengwa wote waliobaki wanafikiwa ndani ya muda uliopangwa ili kufanikisha dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma za afya bila ubaguzi.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vitambulisho hivyo, uongozi wa mkoa ulisisitiza kuwa hatua hii ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuboresha ustawi wa wananchi, kupunguza vifo na magonjwa, na kuondoa mzigo wa gharama za matibabu kwa kaya zisizo na uwezo.

Wanufaika waliokabidhiwa vitambulisho wameishukuru Serikali kwa mpango huu, wakisema utawasaidia kupata matibabu kwa wakati na kuimarisha afya za familia zao.

Serikali inaendelea kutoa wito kwa wananchi wote walengwa ambao bado hawajafikiwa kujitokeza wakati zoezi likiendelea katika maeneo yao, ili kuhakikisha hakuna anayebaki nyuma katika kupata haki ya msingi ya huduma za afya.

**MATUKIO KWA PICHA**





Sehemu ya wananchi wa Wilaya za Hanang na Mbulu wakiwa na kadi za matibabu walizopata kupitia usajili wa Kaya zisizo na uwezo zinazogharamiwa na Serikali

## Singida

# Kaya 7,313 Zisizo na Uwezo Singida zafikiwa Bimaya Afya

Jumla ya Kaya zisizo na uwezo 7,313 zimefanikiwa kufikiwa na mpango Bima ya Afya kwa Wote unaogharamiwa na Serikali. Kaya hizo zenye jumla ya wanufaika 18,524 zimesajiliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu.

Kaya hizo ni sawa ana asilimia 54 ya kati ya Kaya 13,490 zenye jumla ya wanufaika 59,307 zinazolengwa na mpango huo.

Wananchi hao wanatoka katika Manispaa ya Singida, Halmashauri ya Singida, pamoja na Halmashauri za Mkalama, Iramba, Ikungi, Manyoni na Itigi, zikionesha ushiriki mpana wa mamlaka za serikali za mitaa katika kusimamia utekelezaji wa mpango huo muhimu wa kijamii.

Zoezi la usajili na utoaji wa vitambulisho limesimamiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa kushirikiana na Ofisi ya Serikali ya Mkoa, ambapo timu za wataalamu zilifika hadi ngazi ya kata, mitaa na kaya za wanufaika kwa ajili ya uhakiki wa taarifa na utengenezaji wa vitambulisho papo hapo.

Hatua hiyo imeongeza ufanisi na kuhakikisha walengwa wanafikiwa kwa wakati, hususan kaya zenye uhitaji maalum, na hivyo kupunguza changamoto ya gharama za matibabu kwa wananchi wa kipato cha chini.

Utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote unaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa usawa, ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora za matibabu bila kuathiri hali yake ya kiuchumi.

**MATUKIO KWA PICHA**









Sehemu ya Wazee kutoka Kijiji cha Sukamahela, Manyoni wakionesha kadi za matibabu walizopata kupitia mpango wa usajili wa Kaya sizizo na uwezo

# Kigoma

## Asilimia 66 ya Kaya Zisizo na Uwezo Kigoma Zasajiliwa Bima ya Afya

● ***Kunufaika na matibabu bila kikwazo cha fedha***

Jumla ya Kaya 9,968 kati ya Kaya 15,002 sawa na asilimia 66 katika Mkoa wa Kigoma zimefikiwa na kusajiliwa katika mpango unaogharamiwa na Serikali wa Bima ya Afya kwa kaya zisizo na uwezo.

Kaya za walengwa mkoani humo zina jumla ya wanufaika 66,088 ambao walitambuliwa na wamelengwa kufikiwa na mpango huo ambapo mpaka sasa ni wanufaika 28,009 tu ndio wamefikiwa na kupewa vitambulisho vya matibabu.

Ofisi ya NHIF Kigoma kwa kushirikiana na viongozi wa Mkoa kwa kushirikiana na Watendaji wa Halmashauri, Kata na vijiji wameendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa ajili ya kusajiliwa ili wanufaike na mpango huo unaogharamiwa na Serikali.

**MATUKIO KWA PICHA**







Wakazi wa Kijiji cha Ruyenzi, Kata ya Kiziguzigu, Wilaya ya Kakonko wakisajiliwa na kupatiwa bima ya afya kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

# Tanga

## Kaya 13,100 Zisizo na Uwezo Tanga zasajiliwa bima ya afya

Jumla ya Kaya 7,466 kati ya Kaya 13,100 sawa na asilimia 57 zimesajiliwa na kupatiwa vitambulisho vya matibabu kupitia mpango wa Bima ya Afya unaogharamiwa na Serikali.

Mkoa wa Tanga umelenga kusajili kaya 13,100 zenye wanufaika 56,839 ambapo mpaka sasa asilimia 57 ya kaya zote ndio imefikiwa ikiwa na wanufaika 16,830.

Kupitia kadi hizo, kaya wanufaika hao wanaweza kupata huduma za matibabu katika vituo vya afya vilivyosajiliwa bila ya kikwazo cha fedha.

Serikali imeendelea kusisitiza dhamira yake ya kufikia asilimia 100 ya walengwa waliotambuliwa, na hivyo kuhakikisha hakuna kaya zisizo na uwezo inayosalia bila kinga ya matibabu. Mkoa wa Tanga umejipanga kuongeza kasi ya utekelezaji katika kipindi kijacho ili kufikia malengo hayo kwa wakati.

**MATUKIO KWA PICHA**







Wakazi wa Kijiji cha Mzundu, Kata ya Ndolwa,-Wilaya ya Handeni wakielimishwa kuhusu bima ya afya kwa wote na kupatiwa kadi za bima ya afya

## Katavi

# Asilimia 55 ya Kaya Zisizo na Uwezo Zafikiwa Katavi

● ***Wasajiliwa na Bima ya Afya***

Katika utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote unaolenga Kaya Zisizo na uwezo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umefanikiwa kusajili jumla ya kaya 2,901 zenye wanufaika 8,000.

Kwa mujibu wa zoezi la utambuzi wa Kaya Zisizo na uwezo lililofanyika mkoani humo, jumla ya kaya 5,261 zenye wanufaika 23,236 ndio zililengwa kugaharamiwa na Serikali kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa wote.

Akizungumzia hatua iliyofikiwa na mikakati inayoendelea, Meneja wa NHIF Mkoa wa Katavi, Bw. Ally Mwakababu, alisema kuwa usajili unaendelea katika Halmashauri zote tano za Mkoa huo ambazo ni Mpanda, Msimbo, Mpimbwe, Mlele na Tanganyika.

Alisema NHIF inaendelea kushirikiana kwa karibu na uongozi wa Serikali kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Serikali za Mitaa na Vijiji ili kuhakikisha walengwa wote wanafikiwa na kusajiliwa kwa asilimia 100.

"Tunashirikiana na uongozi wa Serikali kuanzia ngazi ya Mkoa hadi Serikali ya Mtaa au Kijiji na tumekubaliana ni lazima tuwafikie walengwa na kuwasajili kwa asilimia 100. Hivyo tunaendelea na jitihada hizi ili lengo la Serikali la kuwalipia wananchi wasio na uwezo liweze kufikiwa," alisema Bw. Mwakababu.

Utekelezaji wa mpango huo umeendelea kuleta matumaini mapya kwa wananchi wa Katavi, hususan Kaya Zisizo na uwezo ambazo sasa zinapata fursa ya huduma za matibabu kwa uhakika zaidi. Serikali imekuwa ikisisitiza kuwa afya ni msingi wa maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla, hivyo uwekezaji katika bima ya afya ni hatua muhimu ya kujenga jamii yenye ustawi na tija.

**MATUKIO KWA PICHA**







Wakazi wa Kijiji cha Kilimahewa, Kata ya Shanwe, Manispaa ya Mpanda wakiwa wamepatiwa kadi zao za bima ya afya kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo.

# Kagera

## Kaya 9,908 Zisizo na Uwezo Kagera Zafikiwa

● ***Wapewa kadi za matibabu***

Mkoa wa Kagera umefanikiwa kuzifikia kaya 9,908 kati ya kaya 15,102 zilizolengwa katika mpango wa kugharamiwa huduma za matibabu na Serikali kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa wote.

Mkoa huo una jumla ya walengwa wanufaika 67,752 ambao wametambuliwa ambapo mpaka sasa wanufaika 27,183 ndio wamesajiliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu.

Hatua hiyo inawezesha kaya zisizo na uwezo kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha katika vituo vya afya vilivyosajiliwa. Hata hivyo zoezi la usajili linaendelea ili kuwafikia walengwa wote.

**MATUKIO KWA PICHA**





Wakazi wa Kijiji cha Nyakatale wilayani Kyerwa, Kagera wakionesha kadi za matibabu walizopewa kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa Kaya zisizo na uwezo

## Tabora

# Asilimia 52 ya Kaya Zisizo na Uwezo Tabora zafikiwa Bima ya Afya

Utekelezaji wa Usajili wa Kaya zisizo na uwezo Mkoani Tabora kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, umefanikiwa kufikia jumla ya Kaya 8,229 zenye wanufaika 21,079 kwa kuzisajili na kuzipatia vitambulisho vya matibabu

Wananchi hao waliofikiwa wamesajiliwa na kupewa Vitambulisho vya matibabu ambavyo vimegharamiwa na Serikali kwa ajili ya kuwawezesha kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Hata hivyo, NHIF Tabora kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi ya Mkoa hadi Mtaa wanaendelea na usajili ili kuwafikia walengwa wote na kuondoka adha ya wananchi hao katika upande wa huduma za matibabu.

---

**MATUKIO KWA PICHA**



Wakazi wa kata Igwisi wilaya ya Kaliua wakiwa wamepatiwa kadi zao za bima ya afya katika zoezi la usajili wa kaya zisizo na uwezo lililofanyika wilayani hapo

# Iringa

## Asilimia 66 ya Kaya Zisizo na Uwezo Iringa zafikiwa Bima ya Afya

● ***Ni wanaolipiwa na Serikali***

Katika utekelezaji wa Usajili wa Kaya zisizo na uwezo, Mkoa wa Iringa umefikia jumla ya kaya 2,820 kati ya kaya 4,267 sawa na asilimia 66.

Kaya zilizofikiwa zina jumla ya wanufaika 6,930 kati ya wanufaika wote 18,325 waliotambuliwa na ambao Serikali inagharamia huduma za matibabu.

Usajili huo unawezesha kaya masikini kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha katika vituo vya afya vilivyosajiliwa, hatua inayolenga kupunguza mzigo wa gharama za matibabu kwa familia zenye kipato cha chini.

Viongozi wa mkoa kwa kushirikiana na watendaji wa ngazi za halmashauri, kata na vijiji wameendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa ajili ya usajili, ili kuhakikisha walengwa wote wanafikiwa kwa wakati.

**MATUKIO KWA PICHA**



Wakazi wa kata ya Nyololo wilaya ya Mufindi, wapatiwa kadi za bima ya afya kwa kuanza na kaya zisizo na uwezo.

# Dar es Salaam

## Asalimia 57 ya Kaya Zisizo na Uwezo  Dar es Salaam zasajiliwa Bima ya Afya

Ofisi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Dar es Salaam zimefanikiwa kusajili Kaya zisizo na uwezo 545 kati ya Kaya 950 kwenye mpango wa Bima ya Afya.

Kaya zilizosajiliwa zina jumla ya wanufaika 2,376 kati ya 4,232 ya wanufaika wote waliolengwa kwenye mpango huu ambao gharama zake zinagharamiwa na Serikali.

Wananchi hao wametoka katika Kata 21 kati ya Kata 36 zilizopo Wilaya ya Ilala, huku juhudi zikiendelea kuhakikisha walengwa wote 1,415 wanafikiwa na kunufaika na mpango huo wa Bima ya Afya kwa Wote.

Wananchi waliofikiwa wameeleza kuridhishwa na mpango huo wakisema utasaidia kupunguza mzigo wa gharama za matibabu na kuwapa uhakika wa kupata huduma wanapohitaji.

Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote unaendelea kutekelezwa nchi nzima kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wote, hususan wale wa kipato cha chini, ikiwa ni hatua muhimu katika kuimarisha ustawi wa jamii na maendeleo ya taifa.

**MATUKIO KWA PICHA**






Wakazi wa Kata ya Tabata katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam baada ya kupatiwa kadi za matibabu

# Simiyu

## Asilimia 56 ya Kaya Zisizo na Uwezo zasajiliwa Simiyu

● ***Wananchi 23,034 Wapewa Vitambulisho vya Matibabu***

Wananchi wa Mkoa wa Simiyu wameeleza furaha yao kufuatia utekelezaji wa ahadi ya Samia Suluhu Hassan ya kuwapatia vitambulisho vya matibabu wananchi wanaotoka katika kaya zisizo na uwezo ili waweze kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

Jumla ya wananchi 23,034 kutoka kaya hizo wametambuliwa, kusajiliwa na kupatiwa vitambulisho vya matibabu kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Hatua hiyo imeongeza matumaini kwa kaya zenye uhitaji, hususan katika maeneo ya vijijini, kwa kuwa sasa wana uhakika wa kupata huduma za matibabu katika vituo vilivyosajiliwa.

Zoezi la usajili na utoaji wa vitambulisho limeongozwa na Uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Simiyu kwa kushirikiana na wilaya zote pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Simiyu, ambapo timu za wataalamu zilifika kwa wananchi kwa ajili ya uhakiki na utengenezaji wa vitambulisho.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo katika Wilaya ya Itilima, Mkuu wa Wilaya hiyo, Anna Kidalya, amesema Serikali imetekeleza kwa vitendo ahadi yake ya kugharamia huduma za matibabu kwa wananchi wanaotoka kaya zisizo na uwezo.

"Mhe. Rais aliahidi na sasa ametimiza. Leo tunapokea vitambulisho vya matibabu ambavyo tutavitumia katika vituo vya kutolea huduma za afya ili tupate huduma bila kikwazo cha fedha na kulinda afya zetu," alisema Mkuu huyo wa Wilaya.

Utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote utapunguza mzigo wa gharama za matibabu kwa wananchi wa kipato cha chini na kuhakikisha kila Mtanzania anapata haki ya huduma za matibabu.

**MATUKIO KWA PICHA**





Wakazi wa Kijiji cha Ihayabuyaga, Kata ya Shigala, wapatiwa kadi za bima ya afya kwa kuanza na kaya zisizo na uwezo.

## Shinyanga

# Asilimia 54 ya Kaya Zisizo na Uwezo Shinyanga zasajiliwa Bima ya Afya

Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, hususan wanaotoka katika kaya zisizo na uwezo, wameipongeza Serikali kwa kutimiza ahadi yake ya kuwagharamia huduma za matibabu kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

Kupitia mpango huo, jumla ya Kaya 8,136 sawa na asilimia 54 zimefikiwa kwa kusajiliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu.

Mkoa huo una jumla ya Kaya 14,459 zinazolengwa kugharamiwa na Serikali ambazo zina jumla ya wanufaika 64,219.
Akizungumzia mafanikio ya zoezi hilo, Meneja wa Mkoa wa Shinyanga wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bw. Izaack Katenda, alisema kuwa wananchi waliosajiliwa wanatoka katika kata 60 na vijiji 253 vya mkoa huo.

Alieleza kuwa zoezi la usajili bado linaendelea ili kuwafikia walengwa wote waliotambuliwa, akisisitiza kuwa lengo ni kuhakikisha hakuna kaya zisizo na uwezo inayokosa fursa ya kupata huduma za matibabu.

"Bado tunaendelea na zoezi la kuwafikia wananchi wengine na tutahakikisha walengwa wote wa mpango huu tunawafikia ili kutimiza azma ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya bila changamoto ya fedha," alisema Katenda.

Wananchi waliofikiwa wameeleza kuwa mpango huo umepunguza mzigo wa kifedha kwa familia zao na kuongeza uhakika wa kupata huduma stahiki katika vituo vya afya vilivyosajiliwa.

Utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote unaendelea kuimarika nchini, ukiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali za kufikia huduma bora za afya kwa wananchi wote bila ubaguzi.

**MATUKIO KWA PICHA**





Wakazi wa Kata ya Kitangili Manispaa ya Shinyanga wapatiwa kadi za bima ya afya kwa kuanza na kaya zisizo na uwezo.

# Pwani

## Asilimia 53 za Kaya Zisizo na Uwezo  Pwani zasajiliwa Bima ya Afya

Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mkoa Pwani imefanikiwa kufikia wanufaika kaya 3,288 kati ya kaya 6,206 zenye wanufaika 8,220.

Mkoa huo una jumla ya kaya 6,206 zenye wanufaika 25,686 zimelengwa kufikiwa na kupatiwa vitambulisho vya matibabu. Ambapo mpaka sasa wanufaika waliofikiwa nis awa na asilimia 32.

Ofisi ya NHIF imeshirikiana na Uongozi wa Mkoa huo kuhakikisha wanufaika wanafikiwa ili kufanikisha Ahadi iliyotolewa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuanza utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote hususan kwa Kundi la Kaya zisizo na uwezo.

**MATUKIO KWA PICHA**



Wananchi kata ya Beleni  Wilaya ya Mafia wakiwa wamepatiwa kadi ya bima ya afya

# Morogoro

## Asilimia 70 ya Kaya Zisizo na Uwezo Morogoro zasajiliwa Bima ya Afya

Mkoa wa Morogoro umeendelea kupiga hatua katika utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote unaolipiwa na Serikali, ambapo hadi sasa jumla ya kaya 9,144 sawa na asilimia 70 zimefikiwa kwa kusajiliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu vitakavyowawezesha kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

Kwa mujibu wa takwimu za utekelezaji, Mkoa wa Morogoro una Halmashauri tisa (9) zenye jumla ya wananchi 13,099 zinazolengwa kwenye mpango huu zenye jumla ya wanufaika 55,611 waliotambuliwa kutoka kaya zisizo na uwezo kunufaika na mpango huo wa Serikali. Hadi sasa, usajili umefanyika katika Manispaa ya Morogoro pamoja na Halmashauri za Morogoro Vijijini, Mvomero, Ifakara, Gairo na Kilosa. Hatua hiyo inaashiria dhamira ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha huduma za afya zinawafikia wananchi wote hususan walioko katika mazingira magumu. Kupitia mpango huu, wanufaika wanapatiwa vitambulisho vya matibabu vinavyowawezesha kupata huduma katika vituo vya afya vilivyosajiliwa bila kulazimika kutoa fedha taslimu wanapohitaji matibabu.


Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Morogoro, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inaendelea na zoezi la usajili kwa wanufaika waliobaki. Lengo ni kuhakikisha walengwa wote 55,611 wanafikiwa na kunufaika na haki yao ya kupata huduma za afya kwa wakati.

Uongozi wa Mkoa umeeleza kuwa ushirikiano unaoendelea kati ya NHIF na Serikali za Wilaya umeongeza kasi ya utekelezaji, huku wananchi wakihamasishwa kujitokeza kuhakiki taarifa zao na kukamilisha usajili. Aidha, viongozi wa ngazi za kata na vijiji wameendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa bima ya afya ya kijamii na namna ya kuitumia mara baada ya kupokea vitambulisho vyao.

Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote unaolipiwa na Serikali ni sehemu ya juhudi za kuimarisha ustawi wa jamii na kupunguza mzigo wa gharama za matibabu kwa kaya zisizo na uwezo. Kupitia utekelezaji wake, Mkoa wa Morogoro unatarajia kufikia asilimia 100 ya walengwa katika kipindi kijacho, hatua itakayochochea upatikanaji wa huduma bora za afya na kuimarisha maendeleo ya wananchi wake.

**MATUKIO KWA PICHA**





Wanufaika kutoka Wilaya ya Morogoro Vijijini wapatiwa kadi za bima ya afya kwa kuanza na kaya zisizo na uwezo.

## Geita

# Asilimia 64 ya Kaya Zisizo na Uwezo zafikiwa Bima ya Afya kwa Wote

Mkoa wa Geita umefanikiwa kuzifikia Kaya 9,964 sawa na asilimia 64 ya Kaya zote 15,623 zinazolengwa kusajiliwa na kupewa vitambulisho vya matgibabu kupitia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Kwa mujibu wa takwimu za mkoa, Geita ina jumla ya wanufaika 69,652 ambapo mpaka sasa jumla ya wanufaika 29,849 wamefikiwa na kupewa vitambulisho vya matibabu.

Katika kuimarisha utekelezaji huo, uongozi wa Serikali ya Mkoa wa Geita umeweka mkakati wa kusajili walengwa kwa asilimia 100 ili kila kaya zisizo na uwezo ipate fursa ya kupata matibabu kupitia bima hiyo ya kijamii.

Akizungumza katika kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mpango huo, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Hashim Komba, aliwataka viongozi wa ngazi zote kusimamia kikamilifu zoezi la usajili katika maeneo yao ili kuhakikisha hakuna kaya zisizo na uwezo inayokosa fursa hiyo muhimu.

Alieleza kuwa zoezi hilo ni utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma za matibabu kupitia mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote, huku Serikali ikigharamia gharama za matibabu kwa kaya zisizo na uwezo.

"Suala la matibabu ni muhimu sana kwa wananchi wetu. Tuhakikishe wanaitumia fursa hii kwa kuwa Serikali yao tayari imeshalipa fedha kwa ajili ya kugharamia matibabu yao. Zoezi hili ni bure, hivyo asiwepo mtu wa kuleta ulaghai wa aina yoyote," alisisitiza Mhe. Komba.

Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote unatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika upatikanaji wa huduma za afya, hasa kwa makundi yenye uhitaji maalum, kwa kuondoa kikwazo cha gharama na kuongeza usawa katika huduma za matibabu kwa wananchi wa Mkoa wa Geita.

**MATUKIO KWA PICHA**





Wakazi wa Kata ya Nyijundu, Wilaya ya Nyang'wale wapatiwa kadi za bima ya afya kwa kuanza na kaya zisizo na uwezo.

## Dodoma

# Bima ya Afya Kwa Wote Yaacha Kicheko Dodoma

- ***Asilimia 74 ya Kaya Zasajiliwa***

Mkoa wa Dodoma kupitia utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, umesajili Kaya 7,904 sawa na asilimia 74 ambayo kati ya kaya 10,723 zilizolengwa kulipiwa gharama za matibabu kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa wote.

Kaya zilizolengwa zina jumla ya wanufaika 46,515 ambapo mpaka sasa waliosajiliwa ni wanufaika 21,183.

Utekelezaji huo ni sehemu ya kutimiza ahadi ya Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kaya zisizo na uwezo zinapatiwa huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha. Hatua hiyo imeanza kuleta matumaini mapya kwa maelfu ya familia zinazokwenda kunufaika na huduma hizo.

Wananchi waliopatiwa kadi hizo wameeleza kuwa mpango huo utasaidia kupunguza mzigo wa gharama za matibabu na kuwapa uhakika wa kupata huduma katika vituo vya afya vilivyosajiliwa bila wasiwasi wa fedha.

Usajili unaendelea katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo kwa kushirikiana na viongozi.

Ofisi ya NHIF Mkoa wa Dodoma umejipanga kuongeza kasi ya utekelezaji ili kufikia asilimia 100 ya kaya na wanufaika waliokusudiwa, na hivyo kuhakikisha hakuna kaya

**MATUKIO KWA PICHA**



Wakazi wa Wilaya ya Mpwapwa wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

# Arusha

## Asilimia 43 ya Kaya Zisizo na Uwezo  Arusha zasajiliwa Bima ya Afya

Mkoa wa Arusha umeendelea kutekeleza kwa vitendo Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, ambapo hadi sasa kaya 5,495 kati ya kaya 12,714 zilizolengwa zimehakikiwa na kusajiliwa sawa na asilimia 43 ya utekelezaji.

Takwimu hizo zinaonesha jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali katika kuhakikisha kaya zisizo na uwezo zinapatiwa kinga ya gharama za matibabu kupitia mpango huo unaogharamiwa kikamilifu na Serikali.

Kwa upande wa wanufaika, mkoa huo ulikuwa na lengo la kuwafikia wananchi 56,715 kutoka kwenye kaya hizo. Hadi sasa jumla ya wanufaika 12,574 wamehakikiwa na kupatiwa kadi za matibabu.

Utekelezaji huo ni sehemu ya dhamira ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wote, hususan wale wa kipato cha chini, wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

**MATUKIO KWA PICHA**





Wanufaika kutoka Wilaya ya Karatu wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

## Ruvuma

# Kaya 5,154 zisizo na uwezo Ruvuma zasajiliwa Bima ya Afya

- ***Ni kupitia Bima ya Afya kwa Wote***

Mkoa wa Ruvuma umeendelea kutekeleza kwa vitendo Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, unaolenga kuwapatia kaya masikini huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Kwa mujibu wa takwimu za utekelezaji, mkoa huo ulilenga kusajili kaya 11,306 ambapo hadi sasa umefanikiwa kusajili kaya 5,154 sawa na asilimia 46 ya utekelezaji.

Idadi ya wanufaika wote mkoani humo ni 51,166 ambao walitambuliwa kunufaika na mpango wa Bima ya Afya wanaolipiwa na Serikali. Hata hivyo mpaka sasa jumla ya wanufaika 15,662 ndio wamefikiwa na kupewa vitambulisho vya atibabu.

Kupitia kadi hizo, kaya masikini zinaweza kupata huduma za matibabu katika vituo vya afya vilivyosajiliwa wakati wowote bila kikwazo cha fedha.

**MATUKIO KWA PICHA**







Wakazi wa Kata ya Maweso, Wilaya ya Madaba, Mkoa wa Ruvuma wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

## Rukwa

# Asilimia 66 ya Kaya Zisizo na Uwezo Rukwa Zasajiliwa Bima ya Afya

Katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote ambao umeanza na Kundi la Kaya Masikini zinazogharamiwa na Serikali, Mkoa wa Rukwa umefanikiwa kusajili asilimia 66 ya kaya zote zilizolengwa na mpango huo.

Mkoa huo una jumla ya Kaya masikini 10,739 ambapo mpaka sasa Kaya zilizosajiliwa ni 7,085 zenye jumla ya wanufaika 21,773 ambao tayari wamepewa vitambulisho vya matibabu vinavyowawezesha kupata huduma bila kikwazo cha fedha.

Ofisi ya NHIF Rukwa kwa kushirikiana na viongozi wa Mkoa na Watendaji wa Halmashauri, Kata na vijiji wameendelea kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa ajili ya kusajiliwa ili wanufaike na mpango huo unaogharamiwa na Serikali.

**MATUKIO KWA PICHA**








Wakazi wa Kata ya Msua, Wilaya ya Sumbawanga Mjini wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

# Lindi

## Kaya 1,570 zisizo na uwezo Lindi zasajiliwa Bima ya Afya

- ***Wanufaika 5,738 wapewa vitambulisho vya matibabu***

Ofisi Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mkoa wa Lindi imetekeleza zoezi la usajili wa kaya masikini kwenye mpango wa Bima ya Afya kwa Wote ili waweze kunufaika na huduma za matibabu wakati wowote.

Utekelezaji huo umezifikia Kaya 1,570 kati ya kaya 4,807 zilizolengwa kufikiwa na mpango huo. Kaya hizo zina jumla ya wanufaika 20,086 na waliosajiliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu mpaka sasa ni 5,738 sawa na asilimia 29.

Mkoa huo unaendelea na umeweka mikakati ya kufikia walengwa wote ili kutimiza maelekezo ya Serikali ya wananchi hao masikini kusajiliwa na kupata huduma za matibabu bure.

---

**MATUKIO KWA PICHA**





Wanufaika kutoka Wilaya ya Kilwa wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

# Mwanza

## Asilimia 71 ya Kaya Zisizo na Uwezo Mwanza zasajiliwa Bima ya Afya

● ***Huduma zake kugharamiwa na Serikali***

Jumla ya Kaya masikini 13,622 kati ya kaya 19,292 sawa na asilimia 71 zimefikiwa na kusajiliwa katika mpango wa bima ya Afya unaogaharamiwa na Serikali ilikuwawezesha wanawake hao kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Mpaka sasa jumla ya wanufaikia 38,557 kati ya 85,487 wamesajiliwa na kupatiwa vitambulisho vya matibabu vitakavyowawezesha kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma bila kikwazo cha fedha.

Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na Viongozi mbalimbali wa ngazi ya Mkoa hadi ngazi ya Mtaa wanaendelea na zoezi hilo ili kuwafikia wanufaika wote mkoani humo.

**MATUKIO KWA PICHA**



Wakazi wa Wilaya ya Kwimba wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

# Njombe

## Njombe kuwa na Uhakika wa Matibabu

● ***Wanufaika 5,495 wapata vitambulisho vya Matibabu***

Kuanza kutekelezwa kwa mpango wa Serikali wa kugharamia wananchi wanaotoka Kaya zisizo na uwezo umepokelewa kwa matumaini makubwa kwa kuwa unakwenda kuondoa tatizo la wananchi hao kukosa huduma za matibabu kutokana na kushindwa kumudu gharama za matibabu.

Katika Mkoa wa Njombe zoezi la kuzifikia Kaya masikini na kuzisajili linaendelea ambapo mpaka sasa jumla ya Kaya 2,307 zimefikiwa zenye wanufaika 5,495 .

Wananchi ambao wamesajili tayari wamepata vitambulisho vya matibabu ambavyo vitawawezesha kupata huduma za matibabu wakati wowote kwenye vituo vya kutolea huduma.

**MATUKIO KWA PICHA**





Wakazi wa Kata ya Mlangali, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

# Songwe

## Songwe wafikiwa Bima ya Afya kwa Wote

- ***Asilimia 42 ya Kaya masikini zafikiwa wa mpango Bima ya Afya kwa Wote***

Mkoa wa Songwe ni moja ya Mikoa itakayonufaika na Mpango wa Serikali wa kuzilipia Kaya masikini gharama za matibabu kupitia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Mkoa huo una jumla ya Kaya kaya 4,867 zilizotambuliwa na kulengwa kugharamiwa ambapo mpaka sasa kaya 2,062 sawa na asilimia 42 ya kaya hizo.

Kutokana na hiyo, jumla ya wanufaika 4,769 wamesajiliwa na kupewa vitambulisho vya matibabu ambapo watanufaika na huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Serikali ya awamu ya sita imetimiza ahadi yake ya kugharamia huduma za matibabu kwa kaya masikini kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Wananchi hawa watakuwa na uhakika wa kupata huduma wakati wowote bila kikwazo cha fedha.

**MATUKIO KWA PICHA**







Wakazi wa Kijiji cha Nseketwa, Kata ya Ihanda, Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

## Mbeya

# Asilimia 60 ya Kaya Zisizo na Uwezo Mbeya zasajiliwa Bima ya Afya

Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Mkoa wa Mbeya umefanikiwa kusajili jumla ya Kaya Masikini 4,753 sawa na wanufaika 12,698 ambao watanufaika na huduma za matibabu bure kupitia vituo mbalimbali vilivyosajiliwa.

Mkoa wa Mbeya una jumla ya Kaya 7,912 ambazo zimetambuliwa na zitanufaika na mpango wa Bima ya Afya kwa kupatiwa vitambulisho vya matibabu vitakavyowawezesha kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Mpango huo unaoratibiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unalenga kuhakikisha wananchi wanaotoka katika kaya masikini wanapata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha, kwa gharama kulipiwa na Serikali.

**MATUKIO KWA PICHA**







Wakazi wa Kijiji cha Ntandabala, Kata ya Masoko, Wilaya ya Rungwe wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

**Mtwara**

# Asilimia 75 ya Kaya Zisizo na Uwezo Mtwara zasajiliwa Bima ya Afya

● ***Kupata huduma za matibabu bure***

Jumla ya Kaya Masikini 7,647 Mkoa wa Mtwara zimefikiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kusajiliwa na kupewa kadi za matibabu kupitia mpango wa Bima ya Afya.

Mkoa wa Mtwara una jumla ya kaya 10,263 zenye wanufaika 38,963 ambazo zimelengwa kufikiwa na mpango huu ili kuwezesha wananchi hao kupata huduma za matibabu bila kikwazo chochote.

Hata hivyo NHIF Mkoa wa Mtwara kwa kushirikiana na Serikali wamejipanga kuhakikisha wote

**MATUKIO KWA PICHA**





Mkuu wa Wilaya ya Newala, Mhe. Alhaji Rajabu Kundya akikabidhi kadi za bima ya afya kwa Wakazi wa Wilaya hiyo

## Kilimanjaro

# Asilimia 62 ya Kaya Zisizo na Uwezo Kilimanjaro Zafikiwa Bima ya Afya kwa Wote

Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Mkoa wa Kilimanjaro imefanikiwa kuzifikia Kaya 4,097 kati ya Kaya 6,650 zilizoko kwenye mpango wa kugharamiwa huduma za matibabu na Serikali kupitia Bima ya Afya kwa Wote.

Wanufaika ambao wamesajiliwa na kupewa vitambulisho mpaka sasa ni 10,275 sawa na asilimia 38 ya wanufaika wote.

**MATUKIO KWA PICHA**





Wakazi wa Wilaya ya Siha wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo

## Mara

# Mara kunufaisha wananchi 17,205 Bima ya Afya kwa Wote

Wananchi 17,205 katika Mkoa wa Mara wamefikiwa na kusajiliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa lengo la kugharamiwa huduma za matibabu na Serikali. Ofisi za NHIF zilizopo Mkoa wa Mara, zinaendelea kushikirikiana na viongozi wa Serikali ngazi zote ili kuhakikisha usajili unakuwa wa asilimia 100.

**MATUKIO KWA PICHA**







Wakazi wa Kata Kiriba, kijiji cha Bwaikwitururu Wilaya ya Musoma Vijijini wakiwa na kadi zao za Bima ya Afya baada ya usajili kupitia mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kaya zisizo na uwezo